TANGAZO LA SERIKALI Na. 861 la tarehe. 18/10/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MASOKO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA-MIKINDANI YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 220 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Masoko ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Masoko ya Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ya Mwaka 2024, ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya kanuni ya 3

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kuongeza maneno “na Mkurugenzi” mara baada ya neno “atakayeteuliwa” linaloonekana katika tafsiri ya neno “Afisa Mwidhiniwa”.

Marekebisho ya kanuni ya 5

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 5, kwa-

(a) kufuta kanuni ndogo ya (3) na badala ya kuweka kanuni ifuatayo:

“(3) Wajumbe wa kamati ya wadau wa soko watapatikana baada ya kuomba kugombea nafasi hizo katika uchaguzi mkuu wa soko na kupigiwa kura na wafanyabiashara waliopo kwenye rejesta ya soko.”;

(b) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (3), kanuni ndogo zifuatazo:

“(4) Wawakilishi waliotajwa katika kanuni ndogo ya (2) watapatikana baada ya

kila kikundi kuchagua mwakilishi mmoja ambaye jina lake litawasilishwa katika uchaguzi mkuu wa soko kwa ajili ya kupigiwa kura na wafanyabiashara wote wa soko waliopo kwenye rejesta ya soko.

(5) Baada ya kupigiwa kura wawakilishi watatu watakaopata kura nyingi ndiyo watakuwa wawakilishi katika kamati ya wadau wa soko.";

(c) kufuta kanuni ndogo ya (4); na

(d) kupanga upya mtiririko wa kanuni ndogo ya (5) na (6) kuwa kanuni ndogo ya (6) na (7) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 15

**4**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 15(1) kwa kufuta neno "mbili" na badala yake kuweka neno "moja".

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*